Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.29 - 2023*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






## Dar es Salaam DECLARATION on Africa Heads of State Human Capital Summit 26th July 2023

# - KAZI IENDELEE -




## BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
***Kamishna wa Elimu***

Atupele Mwambene
***Mkurugenzi wa Sera na Mipango***

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

Nelly Mtema
***Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja
Veronica Chitunda

**Mawasiliano**:
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## Tunakwende na mabadiliko ya Kisayansi na Teknolojia katika Elimu

Katika ulimwengu wa sasa, haitakuwa rahisi kwa nchi au hata taasisi yoyote kuendelea bila kuzingatia Sayansi na Teknolojia. Imekuwa ni nyenzo kuu katika mawasiliano kuanzia ya kirafiki, kifamilia na hatimae katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo.


Mabadiliko yake yamekuwa ni ya haraka na hivyo kubadili mifumo mingi kwa haraka hivyo na nchi nazo kulingana na hatua za maendeleo zimekuwa zikipokea mabadiliko hayo kwa kasi tofauti. Kikubwa ni kuwa matumizi ya SAYANSI NA TEKNOLOJIA HAYAEPUKIKI. Tanzania imepokea mabadiliko haya na utekelezaji wake kwenda kwa kasi katika sekta zote ikiwemo Elimu.

Hivi sasa katika elimu, teknolojia inawezesha na kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji, imewezesha upatikanaji wa zana za ufundishaji, machapisho na vitabu lakini pia ufanyaji tafiti. Imerahisisha mawasiliano kati ya Mwalimu na Mwanafunzi hususan katika vyuo. Kazi iliyo mbele ni kuhakikisha kunakuwa na madarasa ya kisasa yenye vifaa "smart classes" na huu ndio mwelekeo.

Matumizi ya teknolojia darasani yamerahisisha na kuimarisha mbinu ufundishaji. Mwalimu wa Tanzania leo anatumia kishkwambi na katika baadhi ya shule na vyuo "projectors" zipo kuonesha kinachofundishwa. Hapa hatuwezi pita bila kutoa kongole kwa Rais Wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kupatikana vifaa hivi yaani Vishkwambi. Kongole pia kwa Waziri, Makatibu Wakuu na watumishi wa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kwa kulipa suala hili kipaumbele na kufanikisha. Kila Mwalimu Mkufunzi, Mthibiti ubora wa Shule, Afisa elimu kata ana kishkwambi. Matarajio ni ufanisi zaidi katika kuleta matokeo bora ya elimu.

Lakini pia matumizi haya yanaenda sambamba na kuimarisha ushirikiano na Nchi mbalimbali wadau wa maendeleo katika kufanikisha azma ya kuwa na walimu na wanasayansi na mazingira sahihi ya kufundisha na kujifunza katika masomo ya sayansi na hisabati. Julai 18, 2023 Tanzania na Hungary zilisaini makubaliano ya ushirikiano katika Sekta ya Elimu. Makubaliano hayo yalisainiwa na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda na Waziri wa Nchi ya Hungary Tristant Azbej na kushuhudiwa na Rais wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan na Rais Hungary, Mhe. Hungary Katalin Novak.

Makubaliano hayo yanalenga kuimarisha ufadhili wa masomo kwa Watanzania katika fani za Sayansi, Hisabati, Teknolojia na Mawasiliano ikiwa ni muendelezo wa ushirikiano mzuri wa muda mrefu ambao Tanzania na Hungary zimekuwa nao katika nyanja za Kidiplomasia, Uchumi na Biashara. Heko Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuimarisha diplomasia ya nchi na kuwezesha nchi kufaidika katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu.



Uboreshaji Rasilimali Watu>



# Dar es Salaam Declaration on Africa Heads of State Human Capital Summit 26th July 2023

We, the Heads of State and Governments hosted by the Government of Tanzania, met in Dar es Salaam United Republic of Tanzania on 26th July 2023 for the Africa Heads of State Human Capital Summit.

We thank Her Excellency Dr. Samia Suluhu Hassan President of the United Republic of Tanzania for championing this cause and hosting this important summit to discuss policy priorities, challenges, important objectives, and commitment to invest in our people, specifically on learning, skills, health and innovation to fully realize the demographic dividend of our nations.

We recognize and appreciate the support of the World Bank and other development partners of our countries on the implementation of Agenda 2063: The Africa we want and Agenda 2030 on Sustainable Development to realize improved well- being of our people.







We welcome to the world bank Group's engagement model for promoting a collaborative spirit manifested by understanding and sharing challenges to better support governments in the implementation of their national strategies, through financing instruments adapted to their needs, as demonstrated through the Abidjan initiative. We also recognize the important role existing partnerships play in supporting countries to catalyze more financing for human capital outcomes to further support the partnership.

We note with concern the negative impact caused by climate change COVID 19 pandemic, The Russian Ukraine war on human Capital development particularly in African Countries.

We acknowledge with appreciation the efforts being made by many African Governments towards improving the state of human development, including through increasing national budgetary allocation to education, health, food security and nutrition.

We agreed to consider the "Dar es Salaam Declaration on Africa Heads of State Human Capital Summit" in prioritizing government and development partners' interventions in the coming years on Human Capital Development.

Recognizing that quality education and skills development are essential foundations for human capital development, we commit to increasing investments in education systems, from early childhood education to tertiary and vocational training, to ensure equitable access and improved learning outcomes. We will prioritize the development of foundational skills and relevant skills for the future of work, entrepreneurship and innovation, fostering a culture of lifelong learning. Thus we commit to increasing accessibility, affordability and to ensure quality education as well as reducing learning poverty in our countries by at least a quarter by 2030 and improving literacy rates to reach 75% by 2030

Miundombinu Elimu ya Juu >

# Kigoma wapongeza Serikali kutenga Sh. billioni 36 kujenga tawi la Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS)




Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango amewataka walimu kote nchini pamoja na kazi nzuri wanayoifanya kuendelea kufanya kazi kwa weledi na kujituma.

Makamu wa Rais ametoa agizo hilo wilayani Buhigwe Mkoani Kigoma alipokuwa akipokea madarasa 3, ofisi 2 yaliyokarabatiwa na Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB) pamoja na ununuzi wa madawati 25, computer na photocopier.

Aidha Mhe. Mpango amewataka Wazazi kupeleka watoto shule na kuhakikisha wanasoma. Amesema Rais amefanya uamuzi wa kijasiri kuondoa ada kuanzia elimu ya Msingi hadi kidato cha sita hivyo watoto wasiachwe nyumbani bila kwenda shule.

"Acheni mabinti wasome wamalize tusiharakishe kuwaoza watoto wadogo, hatutapata madaktari, maprofesa,"amesema Dkt. Mpango

Na kuongeza "Kuanzia mwaka huu kwenye shule hii niliyosoma ya Muyama nitaanzisha tuzo ya mwanafunzi bora atakaepata ufaulu mzuri atapata Sh milioni moja, mwanafunzi bora wa kike milioni moja na mwalimu atakaefaulisha katika masomo anayofundisha vivyohivyo,"amesema Dkt. Mpango.

Amewataka wadau wengine kuiunga mkono Serikali katika kuboresha mazingira ya ufundishaji na kujifunzia hasa katika maeneo ya Vijijini.

Nae Mkuu wa Mkoa wa Kigoma Kamishna Thobias Andengenye amesema Mkoa ulipokea Sh bilioni 53.7 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya elimu pamoja na utoaji wa elimu bila ada.

Ameishukuru Serikali pia kuuletea mkoa huo fedha kwa ajili ya ujenzi wa VETA kila Wilaya, ujenzi wa Chuo cha TIA eneo la Kabanga na kutenga Sh. Bilioni 36 kwa ajili ya kuanza ujenzi Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi tawi la Muhimbili.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Buhigwe Mhe. Esau Ngoloka amesema Shule ya Msingi Muyama katika vipindi tofauti ilipokea fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Shule hiyo ikiwemo Sh. Milioni 210 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la wanafunzi wenye mahitaji maalumu, Sh. Milioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa uzio na Sh. milioni 100 kwa ajili ya ukarabati wa vyumba vitatu vya madarasa na ofisi mbili.

Afisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Biashara ya Tanzania (TCB) Sabasaba Moshingi amesema Benki hiyo imejiwekea utaratibu wa kurejesha kwenye jamii na kwamba ukarabati wa madarasa 3 ofisi 2, ununuzi wa madawati 25, computer na photocopier vyote vikitumia Sh Milioni 78 ni sehemu ya utekelezaji wa lengo hilo ambalo benki imejiwekea.

Uimarishaji Elimu ya Stadi za Ufundi >



# Tanzania na China zajipanga kuwanoa vijana stadi za ufundi




aziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali imedhamiria kuimarisha Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kuwawezesha wahitimu kuwa na viwango vya kuajirika Kitaifa na Kimataifa.

Prof. Mkenda ametoa kauli hiyo Kibaha mkoani Pwani, wakati akifungua Kongamano kuhusu ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na China katika masuala ya Elimu ya Ufundi.

"Semina hii inaendana na mipango ya Serikali kupitia Sera mpya yenye mageuzi makubwa ambayo inaifanya elimu ya Ufundi Stadi sasa kuanza kutolewa kuanzia ngazi ya Elimu ya Sekondari, kwa kufanya hivyo vijana wengi wa kitanzania watakuwa na ujuzi na utayari wa kufanya kazi za kuajiriwa au kujiajiri," alisema Prof. Mkenda.

Ameongeza kuwa ushirikiano wa nchi hizo mbili utaisaidia Tanzania kufikia haraka maendeleo ya kiuchumi, kwani China ina mifumo imara katika mafunzo ya Ufundi, Uhandisi.

"Tuna kazi kubwa sana kujifunza kutoka China, wenzetu wana utaalam angalia mafundi wao wanaokuja kusimamia kazi. Hivyo tunahitaji mafundi wetu wawe na uwezo wa kufanya kazi vizuri kama wao," amebainisha Prof. Mkenda.

Akizungumzia matokeo ya ushirikiano huo, Prof. Mkenda amesema tayari Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) imeanzisha program ya shahada ya miaka Minne, ambapo wanafunzi watakaochukuliwa mwaka wa kwanza watasoma hapa Tanzania, miaka miwili watasoma China, halafu watarudi hapa mwaka mmoja, na hivyo watapata shahada ya hapa Tanzania, pamoja na diploma ya China.

"Tumeanza na Wanafunzi 30, sasa hivi wamepelekwa China kufanya mafunzo kwa vitendo, watarudi watasoma na baadae tena watarudi China," amefafanua Prof. Mkenda.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji wa Baraza la Taifa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) Dkt. Adolf Rutayuga amesema hatua ya mashirikiano hayo, ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Serikali, kuunganisha Vyuo vya Kati vya hapa nchini na vile vya Nchi zililoendelea kiteknolojia katika Elimu ya Ufundi.

Amesema vijana watakaopata fursa katika mpango huo wataleta chachu na msingi wa maendeleo ya kiuchumi kwani watakuwa na ujuzi katika viwango vinavyohitaji kimataifa.

Kongamano hilo limezihusisha Taasisi zinazotoa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (TVET) kutoka Tanzania na China, pamoja na Wawakilishi 25 kutoka Fungamano la China-Africa-Alliance ambalo linakuza ushirikiano wa Taasisi za Mafunzo hayo Barani Africa.

Mikopo ya Elimu ya Juu >

# Mwongozo uombaji mikopo Elimu ya Juu 2023/24 wazinduliwa

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga amesema Elimu ni nyenzo muhimu sana katika Maendeleo, kwa kutambua hilo Serikali ipo kwenye hatua mbalimbali za mageuzi, ikiwa ni pamoja na kuimarisha mfumo wa Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Mhe. Kipanga ametoa kauli hiyo jijini Dar es Salaam Julai 13, 2023 akizindua rasmi Mwongozo wa uombaji Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2023/2024.

Mwongozo huo unaelekeza maombi kufanyika kwa njia ya mtandao na dirisha litakuwa wazi kuanzia Julai 15 mpaka Oktoba 15, 2023.

Mhe. Kipanga ameongeza kuwa ingawa Mwongozo huo utapatikana kuanzia tarehe ilipotangazwa, Wanafunzi, wazazi na walezi watapaswa kutumia siku hizi mbili kuusoma na kuzingatia kabla ya kuanza kuomba.

"Katika Mwongozo huo waombaji mkopo hawata tuma nakala ngumu wala kuja Bodi ya Mikopo badala yake watatuma nakala laini, hii ni kutokana na maboresho makubwa ya mfumo wa uombaji yaliyofanywa kupitia ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Juu Kwa mageuzi ya Kiuchumi (HEET)," alisema Mhe. Kipanga.

Aidha ili kurahisisha zoezi la malipo Mhe. Kipanga amesema Mwongozo unamtaka muombaji kufungua akaunti ya SIPA (Student's Individual Permanent Account) kwa ajili ya kufuatilia maombi yake ya mkopo, kuwa na Akaunti ya Benki aipendayo pamoja na nambari ya simu iliyosajiliwa.


Pia amewakumbusha kwamba Mwongozo huu hautawahusu waombaji katika ngazi ya Stashahada, kwani taratibu zinaandaliwa na Mwongozo utatolewa hivi karibuni.

Kipanga ameipongeza Bodi hiyo kuandaa maboresho ya mfumo na Mwongozo huo huku akibainisha kuwa Serikali katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita imeongeza bajeti ya fedha za Mikopo ya Elimu kutoka Shilingi Bilioni 570 (2021-2022) hadi Shilingi Bilioni 731 kwa mwaka mpya wa masomo utakaonza Oktoba, 2023.

"Ongezeko hili la fedha limewezesha idadi ya wanufaika wa Mikopo kuongezeka kutoka 177,615 mwaka 2021-2022 hadi wanufaika 205,000 kwa mwaka huu mpya wa masomo," amebainisha Mhe. Kipanga

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi Elimu ya Juu Bw. Abdul-Razak Badru amesema uzinduzi huo unaashiria kufungua dirisha la maombi ya Mkopo, na kwamba Mwongozo huo unapatikana katika tovuti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia www.moe.go.tz pamoja na tovuti ya Bodi hiyo www.heslb.go.tz

Wakizungumza kuhusu hatua hiyo, wanufaika watarajiwa wa Bodi ya Mkopo Bi. Frida Alex na Bw. Shehe Juma wameishukuru Serikali kuendelea kujali mahitaji ya Wanafunzi ikiwa ni pamoja kuongeza fedha ya kujikimu kwa wanufaika.



Uwajibikaji Maendeleo ya Sayansi >




# Prof Mkenda apongeza Kituo cha Sayansi Tanga katika kuchagiza maendeleo

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amekipongeza Kituo cha STEM Inspire kilichopo mkoani Tanga kwa kutumia Teknolojia na vitu vinavyopatikana ndani ya nchi katika kuendeleza masomo ya Sayansi, Teknolojia na ubunifu.

Akizungumza baada ya kutembelea kituo hicho kuona shughuli mbalimbali zinazofanyika Prof. Mkenda amesema kuwa amepata fursa ya kuangalia na kujifunza kuhusu mbinu zinazotumiwa na wataalam hao kumsaidia mjifunzaji kupata uelewa namna Sayansi inavyofanyakazi katika karne hii.

"Hapa nimeona vitu vizuri, kama ambavyo mmeviona, waliniomba nije nitazame nione wanachokifanya na wanataka tusaini hati ya makubaliano na wizara yetu kwa ajili ya ushirikiano.

"Sasa nimeona wanavyofundisha Sayansi kwa kutumia Teknolojia na vitu vinavyopatikana Tanzania, lakini hapa mafunzo yanafanyika kwa vitendo zaidi na huko tunakoenda mbeleni ni muhimu kuzingatia mfumo shirikishi wa ufundishaji wa watoto wetu ili waweze kufikiri na kufanya uvumbuzi wenyewe," alisema Prof. Mkenda

Ameongeza kuwa, Serikali itashirikiana na Kituo hicho ili kuanzisha kituo kingine kikubwa zaidi mkoani Dodoma, kuwapatia nafasi Wakuu wa Mikoa, Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge kutembelea kwa ukaribu kujionea manufaa yake na hatimaye kuongeza msukumo wa ujenzi wa Vituo hivyo nchi nzima.

"Najua haitawafikia Wanafunzi wote, lakini itaanza kuhamasisha, na mbele ya safari kwenye Mitaala mipya itabidi ishuke kwenye Kata, na hatimaye kila shule, kwa sababu vitu karibu vyote vinapatikana kirahisi ndani ya nchi," alieleza Prof. Mkenda

Akieleza kuhusu kazi ya kituo hicho Mwanzilishi mwenza wa Mradi wa STEM Park Inspire Bw. Lwidiko Edward amesema ni kuhakikisha inalea Watoto kutokana na udadisi wa kiasili wa Sayansi mpaka kuwatengeneza kuwa Wanasayansi halisi kwa kutumia mbinu mbalimbali.

Pia ameongeza kuwa kituo kinaandaa mazingira kwa ajili ya kuwapatia hamasa Watoto kusoma na ndio dhana ya kujenga vituo hivyo jijini Dar es Salaam na Tanga pamoja na kuhakikisha watoto wanapata kujifunza ujuzi na fursa za kuendelea na masomo ngazi za juu.

"Kwa sababu nchi zote zilizoendelea karibu asilimia 60 mpaka 70 ya mapato yao ya ndani ya nchi yanatokana na taaluma za sayansi, uhandisi, teknolojia na hesabu na Tanzania ili tufike huko, tunahitaji wanataaluma wengi katika maeneo hayo, kwa hiyo ndio maana tumekuwa tukifanya hivi karibu miaka nane sasa," amefafanua Bw. Lwidiko

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) Dkt. Amos Nungu amesema wanajivunia Mradi huko unaosaidia kujenga umahiri na kuweka mazingira rafiki kwa wototo kujifunza kwa ari kubwa.

Vile vile amebainisha kwamba, Mradi huo umeleta mafanikio ikiwemo baadhi ya Wanafunzi kushiriki na kufanya vizuri katika Mashindano ya Kimataifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) na wengine kufadhiliwa kwa ajili ya kujiendeleza kimasomo.

Ufadhili Elimu Nchini >

# Canada kuongeza takribani Sh. bilioni 93 kufadhili elimu

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameishukuru Serikali ya Canada kutangaza kuongeza ufadhili wa Dolla za Canada milioni 50 takriban shilingi Bilioni 95 za Tanzania kwa ajili ya kufadhili miradi ya Elimu Tanzania.

Prof. Mkenda ametoa shukrani hizo Julai 20, 2023 baada ya Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa na mwenye dhamana ya Shirika la Maendeleo ya Uchumi la Pasifiki wa Canada Mhe. Harjit S. Sajjan, kutangaza ongezeko hilo.

Prof. Mkenda amesema kuwa Dola milioni 25 zitatumika kuwezesha Wasichana kusoma na kukamilisha mzunguko wa Elimu na Dola milioni 25 zitatumika kuendeleza mafunzo ya Amali kwa vijana kuwawezesha kupata ajira.






"Haya ni mafanikio ya Serikali kuendelea kujenga mahusiano mazuri na nchi mbalimbali na Rais wetu amekuwa akifanya kazi kubwa ya kuimarisha mahusiano hayo". Alisema Prof. Mkenda.

Waziri wa Maendeleo ya Kimataifa na mwenye dhamana ya Shirika la Maendeleo ya Uchumi la Pasifiki la Canada Mhe. Harjit Sajjan amesema Serikali ya nchi hiyo imekuwa Mshirika wa muda mrefu wa Tanzania katika Sekta ya elimu na imefanikiwa kuboresha viwango na upatikanaji wa elimu katika Vyuo vya Ualimu na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi katika kusaidia jitihada mbalimbali za Serikali.

"Kwa kushirikiana na Serikali tumewekeza katika mafunzo mathubuti kwa Walimu katika Vyuo 35 vya Ualimu" ambapo kwa miaka 14 Canada imetoa zaidi ya dolla za Canada milioni 250," alibainisha Mhe. Sajjan.

Waziri huyo ameipongeza Serikali ya Tanzania kwa kuruhusu wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali kurejea shuleni, ili kuwawezesha kupata maarifa na Ujuzi hivyo kushiriki katika uchumi.

Ameongeza kuwa uwekezaji katika Elimu hasa mtoto wa kike hubadilisha jamii, huimarisha uchumi na kuchangia jamii kuwa imara zaidi. Hivyo nchi hiyo itaendelea kushirikiana kuendeleza Sekta ya Elimu.

Nae Mkurugenzi Mkuu na Rais wa Taasisi ya Vyuo vya Canada Bi. Denise Amyot amesema program ya Uwezeshaji Kupitia Ujuzi (ESP) inayolenga kuimarisha usawa wa kijinsia katika Elimu inaunganisha Vyuo na Taasisi za Ufundi za Canada na nyingine kutoka nchi Washirika kubadilishana ujuzi kupitia mpango wa "Elimu Kwa Ajira"

Programu nyingine chini ya UNICEF ijulikanayo kama (Every Adolscent Girl Learns) kila Binti asome ni ya uwezeshaji upatikanaji wa fursa za elimu na ujuzi kukuza uwezeshaji na kupata fursa za ajira staha.

Nae Mwakilishi kutoka UNICEF Daniel Baheta amesema Mradi huu utatekelezwa katika mikoa ya Tabora, Songwe, Kigoma pamoja na Zanzibar.

Ufadhili VETA >




# NBC yatoa ufadhili kwa wanafunzi 1,000 VETA




Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imesaini mkataba wa Makubaliano ya ufadhili wa wanafunzi 1,000 wa Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).

Akizungumza jijini Dodoma katika hafla ya utiaji saini Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa ufadhili huo unakwenda kutimiza azma ya Serikali ya kutoa Elimu na Mafunzo yatakayo wawezesha vijana wa kitanzania kupata ujuzi wa kujiajiri ama kuajiriwa.

Prof. Mkenda ameongeza kuwa mageuzi makubwa ya elimu yanayotarajiwa kutokea, yanatilia mkazo mafunzo ya Amali, hivyo Benki hiyo imekuja wakati muafaka kuiunga mkono Serikali katika mpango huo.

"Tumekuwa tukizungumza mafunzo ya amali sana, tunataka tutoe elimu hiyo inayomwezesha kijana kuwa na ujuzi, leo Benki ya NBC imetushika mkono kwenda hatua moja zaidi ya kufanikisha azma hii," amesema Prof. Mkenda

Aidha Waziri Mkenda amewataka wadau wengine kuiunga mkono Serikali kwenye kuimarisha mafunzo na kuongeza fursa katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi - (VETA) na Vyuo vya Kati ili vijana wanufaike na ujuzi utakaopatikana.

Kwa uapnde wake Mkurugenzi Mkuu wa NBC Theobald Sabi amesema kupitia ushirikiano na Wizara, Benki hiyo kwa kuanzia itatoa ufadhili wa Shilingi milioni 100 kwa vijana 1,000 wa VETA kupitia mpango wa " NBC Wajibika Scholarship".

Mkurugenzi Sabi ameongeza kuwa mafunzo yanayo wawezesha vijana kuwa mahiri ndio ufumbuzi wa tatizo la ajira kwa vijana, na hili si hitaji la Tanzania tu bali kwa Dunia nzima.

"Changamoto ya ajira kwa vijana ni kilio cha Dunia nzima, suluhisho thabiti ni kutengeneza mazingira bora kuwawezesha vijana kujiajiri au kujiendeleza kwa kuwa na ujuzi," alibainisha Mkurugenzi Sabi

Nae Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) CPA Anthony Kasore ameishukuru Wizara kwa kuwezesha kupatikana ufadhili huo kutoka Benki ya NBC ambao utawezesha Vyuo hivyo kutoa Mafunzo ya Ujuzi kwa vijana wengi.

Mkurugenzi Kasore amesema kuwa VETA imepokea Mradi huu pamoja na maelekezo ya kuhahakisha zinatumika kwa uwazi na kwa kutoa mafunzo yenye uhitaji na kuleta matokeo chanya kwa haraka.

# Ufundishaji Hisabati kwa TEHAMA >



## Wakufunzi somo la Hisabati wapewa mbinu kufundisha kwa kutumia TEHAMA

Wakufunzi wa somo la Hisabati kutoka Vyuo vya Ualimu vya Serikali wamepatiwa mafunzo kazini juu ya ufundishaji ili kuwapa mbinu bora na mahiri za kufundisha somo hilo kwa kutumia TEHAMA.

Akifungua mafunzo hayo Mkoani Morogoro Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema mafunzo hayo yanalenga pia kuwapa uwezo wakufunzi kuwezeshana kumudu somo hilo hususan kwa njia ya mtandao kupitia kituo cha Umahiri cha Hisabati kilichopo katika Chuo cha Ualimu Morogoro ambacho ni mahsusi kuwahudumia wakufunzi na walimu wa somo la hisabati nchini.

Amesema kumekuwa na changamoto ya ufundishaji wa somo la Hisabati na kuwafanya wanafunzi kutopenda somo hilo na ndio maana Serikali imefanya mafunzo kwa wakufunzi ili kuwapa mbinu za kufundisha kwa kutumia TEHAMA ili kuvutia wanafunzi kupenda kusoma somo hilo.

"Tafiti zimeonesha wanafunzi wengi hawavutiwi kusoma somo la Hisabati na ufaulu kuwa mdogo pengine ni kutokana na namna somo hili linavyofundishwa hivyo mafunzo haya yatawapa mbinu bora za kufundisha na kuwafanya wanafunzi kuelewa na kupenda somo hilo na niseme tu mafunzo haya yahusishe pia wakufunzi kutoka Vyuo vya Ualimu vya binafsi kwa kuwa wanafundisha watoto wa kitanzania kuwa walimu," amesema Prof. Nombo.

Na kuongeza "Tunajua hisabati inatumika katika maisha ya kila siku tunataka wakufunzi hawa waweze kuwezesha walimu tarajali ambao watafundisha shule za msingi na sekondari kutumia hisabati katika maisha ya kila siku lakini kuwezesha wanafunzi kufaulu.

Prof. Nombo amesema utoaji wa mafunzo hayo ni mwendelezo wa mikakati ya Wizara iliyojiwekea kuhakikisha hakuna changamoto za ufundishaji wa somo hilo na hatimaye wanafunzi kupenda kusoma somo hilo.

"Pamoja na kutoa mafunzo kazini tunatoa pia ufadhili wa masomo (Samia Scholarship) kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kwenye masomo ya sayansi wanaomaliza kidato cha sita na kuchagua kendelea na masomo ya sayansi katika fani za tiba, uhandisi na sayansi".

Amesisitiza kuwa Serikali inaendelea na mikakati ya kuvutia wasichana kupenda masomo ya sayansi na hisabati hivyo kuongeza wanafunzi wa kike watakaopenda kufundisha masomo hayo.

Prof. Nombo amemshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuwekeza kwenye Sekta ya elimu ili kutoa elimu iliyo bora.

Aidha ameishukuru Serikali ya Canada kupitia Mradi wa TESP kwa mchango wao mkubwa katika kuendeleza Elimu ya Ualimu nchini kwa kuboresha miundombinu ya Vyuo vya Ualimu, utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu na utaoji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa mafunzo ya Ualimu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Huruma Mageni amesema jumla ya wakufunzi 155 wamepatiwa mafunzo hayo

Ameongeza kuwa mafunzo yanatolewa katika Chuo cha Ualimu Morogoro kwa kuwa Serikali imeanzisha kituo cha umahiri cha hisabati ili kuimarisha na kuendeleza mafunzo ya ufundishaji wa somo hilo katika chuo hicho.

Nae Mratibu wa Mradi wa Kuendeleza Elimu ya Ualimu (TESP) Cosmas Mahenge amesema Mradi umewekeza kwenye masuala ya TEHAMA katika vyuo vya ualimu na sasa unatoa mafunzo ya mbinu za ufundishaji wa somo la Hisabati kwa kutumia TEHAMA ili waendane na mabadiliko yalipo.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakufunzi walioshiriki mafunzo hayo wamesema yatawaimarisha katika ufundishaji hususani matumizi ya TEHAMA na kufanya walimu tarajali wapende somo la hisabati.



Pongezi DIT >



# Dkt. Rwezimula aipongeza DIT usimamizi wa ujenzi kituo cha Umahiri wa TEHAMA

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula ameipongeza Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kwa kusimamia vizuri Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC).

Dkt. Rwezimula ametoa kauli hiyo Jijini Dar es Salaam wakati akifanya ziara katika Taasisi hiyo kushuhudia maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo ambapo amesema kituo hicho kikikamilika kitasaidia nchi kupata wataalam wa masuala ya TEHAMA na kwamba lengo ni kujenga uwezo wa nchi kupata wataalam wenye Ujuzi.

"Serikali yetu ipo kwenye mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 Toleo la 2023 ambapo Mitaala inasisitiza masomo ya sayansi ili mwanafunzi akimaliza elimu ya sekondari awe na Ujuzi wa kutenda. Tunaamini Taasisi ya DIT itakuwa msaada mkubwa katika azma hiyo," amesema Dkt. Rwezimula

Ameongeza kituo hicho kitakapokamilika kitakuwa na fani zitakazoinufaisha nchi Wanachama wa Afrika Mashariki.

"Nimezungumza na wajenzi wameniahidi kwamba watakamilisha Mradi huu kwa wakati, na kwamba ifikapo mwezi Februari 2024 utakuwa umekamilika," alibainisha Dkt. Rwezimula.

Mratibu wa Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa TEHAMA (RAFIC) Dkt. Joseph Matiko amesema Mradi huo mkubwa wa miaka mitano, ulianza mwaka 2019, ambapo Benki ya Dunia imetoa Dola za Marekani milioni 16.25.

"Mradi wa RAFIC wa DIT unajikita katika uimarishaji wa Stadi za kidigital, hapa kuna Stadi za msingi yaani basic skills, kuhakikisha watu wa chini wanaweza kutumia kwa ufanisi vifaa katika shughuli zao kama vile simu. Pia tuna 'standard skills' ambapo zinapeleka Umahiri kwenye mifumo rasmi ya Elimu,"

"Kwa mfano Madaktari, Walimu pia kuna kundi la wabobezi. Wote wanaohusika katika kuimarishiwa umahiri wao kuhusu matumizi ya vifaa vya TEHAMA".



## NUKUU >

**"TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA"**

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifala Elimu ya Ufundi (NACTE),**
S.L.P 7109, DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P. 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz